

MAMLAKA YA MAENEO MAALUM YA UWEKEZAJI (EXPORT PROCESSING ZONES AUTHORITY-EPZA)



TANGAZO KWA WALIPWA FIDIA (ENEO LA EPZA- KURASINI)

MAMLAKA YA MAENEO MAALUM YA UWEKEZAJI (EPZA) ITAANZA AWAMU YA NNE YA ULIPAJI FIDIA KWA WAKAZI WA ENEO LA MRADI WA *KURASINI LOGISTICS CENTRE* KUANZIA TAREHE 05 MEI, 2016. UTARATIBU WA MALIPO, RATIBA NA ORODHA YA NAMBA ZA UTHAMINI ZA WAHUSIKA VIMEBANDIKWA KATIKA MBAO ZA MATANGAZO KWENYE OFISI YA MKUU WA WILAYA YA TEMEKE; HALMASHAURI YA

**MANISPAA YA TEMEKE; OFISI YA KATA YA KURASINI NA
KWENYE MBAO ZA MATANGAZO ZA MAMLAKA YA MAENEO
MAALUM YA UWEKEZAJI (EPZA) NA TOVUTI YA MAMLAKA YA
EPZ www.epza.go.tz .**

**ZOEZI LA MALIPO LITAFANYIKA KATIKA OFISI
ZA MKUU WA WILAYA YA TEMEKE, DAR ES
SALAAM.**

1. MAMBO YA KUZINGATIA KATIKA ZOEZI LA MALIPO:

**I. MALIPO YOTE YATAFANYIKA KWA HUNDI
ILİYOFUNGWA, HIVYO WAHUSIKA WOTE WANATAKIWA
KUWA NA AKAUNTI YA BENKI. AKAUNTI YETU IKO
BENKI YA CRDB.**

**II. KILA MLIPWA FIDIA ANATAKIWA KUHAKIKI MAJINA
YAKE ILI KUHAKIKISHA KWAMBA YANAENDANA NA
NYARAKA ZAKE PAMOJA NA AKAUTI YAKE YA BENKI.
KATIKA KUFANIKISHA ZOEZI HILI MLIPWA FIDIA
ANATAKIWA KUJA NA NYARAKA ZIFUATAZO:**

**(a) KITAMBULISHO HALISI KINACHOTAMBULIKA
KISHERIA HUSUSANI KILE CHA KUPIGIA KURA.**

- (b) NAKALA YA KITAMBULISHO HALISI
KINACHOTAMBULIKA KISHERIA HUSUSANI KILE
CHA KUPIGIA KURA.**
- (c) PICHA TATU ZA RANGI (PASSPORT SIZE)**
- (d) FOMU HALISIA YA MADAI YA FIDIA NAMBA 69
ILİYOTOLEWA NA KAMISHNA WA ARDHI WAKATI
WA ZOEZI LA UTHAMINI.**
- (e) KWA WALE WOTE WANAOSIMAMIA MIRATHI,
WANATAKIWA WAJE NA HATI YA MIRATHI
ILİYOTOLEWA NA MAHAKAMA.**
- (f) YEYOTE ATAKAYE POKEA HUNDI YA FIDIA,
ATATAKIWA KUONDOKA KWENYE ENEO HUSIKA
NDANI YA SIKU SITINI (60) KUPISHA SHUGHULI ZA
MRADI. AIDHA, BAADA YA SIKU SITINI (60)
MAMLAKA ITAANZA ZOEZI LA KUBOMOA NYUMBA
ZILIZOFIDIWA ILI KUANZA UTEKELEZAJI WA
MRADI.**

2. RATIBA YA MALIPO ITAKUA KAMA IFUATAVYO:

TAREHE	TUKIO	WATU WATAKAOLIPWA	MAHALI	MUDA
05/05/2016 ALHAMISI	Malipo ya fidia kwa wakazi wa Kurasini, Mivinjeni,Shimo la Udongo na Kiungani	Wananchi wote waliopo kwenye orodha	Ofisi za Mkuu wa Wilaya ya Temeke.	Saa 3:00 asubuhi hadi Saa 9:00 jioni